Jina: …… Nambari: ……...……

Shule: …… Sahihi .....

Tarehe: ……..……

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA 2
MACHI / APRILI 2011
MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA MUUNGANO KANDA YA BUTERE MASHARIKI

Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)

Kiswahili
Lugha

MAAGIZO

- *Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- *Weka **sahihi yako** na **tarehe** ya mtihnai katika nafasi ulizoachiwa*
- *Jibu maswali yote*
- *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

*Karatasi hii ina kurasa **8** zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

1. UFAHAMU.

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Tulipofika king'ozi tuligundua kuwa safari yetu haingekuwa ya kujivinjari kama tulivyokuwa tumekadiri. Mwenzangu Mbete alikuwa tayari ameanza kuchopea kwa uchovu wa kupiga milundi tangu tulipodamka. Azima yetu ya kuipanga safari hii ilikuwa kutafitia kuhus falsafa ya itikadi ya wana –kotongoji cha king'ozi.

Ni kitongoji kidogo kinachopatikana baina ya mji ya Mgandi na Mlima Kenya. Kitongoji hiki kina sifa kuhifadhi utamaduni na salua au historia yao ndefu ambayo tulinuia kuitafitia.

Tulitaka pia kukutana na wenyeji wa king'ozi ambao sifa ya kuwa na mlahaka usiokuwa na kifani hasa kwa wageni waliozuru katika kijiji hicho. Tulikutana na Mzee ilalo ambaye alitukaribisha kwa mlahaka ambao sijawahi kuuuona aushini mwangu. Alitushauri tuwe na subira hadi mafungulia ng'ombe dnipo tungepata uhondo kamili. Taadhima yake ilituelikeza tusiwe na budi ila kusubiri.

Ilipotimia magharibi tukasikia mlio wa pembe ndipo tukatanabahi kuwa wakati tuliokuwa tumeahidiwa ulikuwa ndio huo. Mzee ilalo akatushauri tusiwe na kiwewe. Tukapiga safari yetu hadi kwenye kina cha msitu mkubwa uliokuwa mkabala na Mlima Kenya. Mara tukasikia nyuma yetu ngoma zikichzwa na kundi kubwa l awatu. Nikatanabahi kuwa baadhi ya nyimbo nilizozisikia zilikuwa kama zile ambazo nilikuwa nimewahi kizisikia kutoka kwa marehemu babu yangu, mojawapo kama "kwani kisu hiki kina nyuki ambao huchoma?" kabla ya kumsaili Mzee Ilalo maana yake, mbete alikuwa amekwishaanza kuingiwa na hatihati kama vile wimbo ulivyoshabihi. Ninavyojua ni kuwa Mbete na nyuki ni kma aliyeumwa n anyoka na ameona ukambaa.

Mzee Ilalo alitushauri tuwe na subira kwani hiyo ilikuwa lele tu. Ghafla bin vuu tukasikia mchakacho karibu nasi. Kutazama nyuma tukaona shababi wakitokea kando kando ya kinjia kidogo kilichokuwa karibu nasi. Walikuwa wanamvalia vinyago na kuonekena kama vigaragosi ambao waliogofya mno.

Kundi la wacheza ngoma lilikuwa tayari limetufikia tukajiunga nao na kuanza kucheza pamoja. Mmjoa wa shababi alikuwa amemburura ngorombwe ghafla. Yule ngorombe akachinjwa na ghalamu. Wakapakwa damu kote kote katika miili yao. Nyama ilichomwa nasi tukapewa kila mmoja pande kubwa la nya ma lililokuwa tamu sana.

Ngoma na miondoo zilianza tena huku kila mmoja akimengua kiuno, ungeohani ni hayawani waliokuwa wakisherehekea nyama ya kiguli. Tulicheza hadi kuku wa kwanza alipowika. Tuliadnamana hadi kwenye chemichemi ya maji yenye mzizimo.

Vijana walijitoma lwenye chemichemi hiyo kukoga hasa damu waliokuwa wame jipaka. Fauka ya kujinadhifisha, maji nayo ya mzizimo yalikuwa na umuhimu mwingin e kma alivyotufahamisha Mzee Ilalo.

Walitoka kwenye chemichemi na kipiga foleni kama Adamu na Awa. Ngoma zilisitishwa tena na kukanyamaa zi! Tukasikia sauti moja kubwa ya kutisha kama ya dume aliyekuwa amepagawa. Baadhi ya vijana hasa wale walioonekna kama wake mbe wakaanza kuwayawaya lakini shinikizo la kuwa walivyotoka kuwa liliwashurutisha kuwa na bila budi ilia kuvumilia na kujizatiti.

Ikanikumbunsha shughuli kama hiyo ambayo nilikuwa nimeshuhudia katika sehemu mo jay a janibu za magharibi mwa Kenya amabapo wanawake walihusika. Pindi nikitafakari nayo,tukajikuta kenye kijia chembamba tulichokuwa tumekipitia n Mzee Ilalo. Nikasikia vigelegele vya wanawake vimetanda katika kijiji kizim acha king'ozi.

Mbete akanining'enezea, "Mbona sikuwaona wanawake wakishiriki kama nilivyokuwa nimewaona katika sehemu za magharibi?". Mzee Ilalo ni kama alikuwa maeyasoma mawazo yetu na ndipo akatujibu haraka. " shughuli hii hairuhusiwi kuwa na wanawake karibu hata?

Tulilala kama tumejivinjari kwa Mzee Ilalo kwa siku mbili baada ya kukamilisha shughuli zetu. Siku ya pili tulipoamka tulimuona mmoja wa wale vijana akiwa ameji jambika kwa shuka nyeupe. Hii ilikuwa tamaduni ambayo waking'ozi walilinzi si haba ili tu kwa wasichana ilikuwa tayari imezikwa katika karibu la sahau kwani ni kuwanyanyasa na kukiuka kanuni zao za kibinadamu.

Mzee Ilalo alitua ga asubuhi ya pili kwa kutuonya kuwa jambo tuliloshuhudia tuliche katika pambizo la msitu na ndipo ni gnependa wewe msomaji usikisome kifungu hiki bali uzuru katika kiji cha king'ozi ujionee mwenyewe mali mwenguni.

Maswali.

1. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (ala.2)
2. Safari hiyo ilikuwa na madhumuni gani kwa mwandishi na mwenzake? (ala.2)
3. Thibitisha kuwa wenyeji wa King'ozi walikuwa na mlhaka mwema. (ala.3)
4. Unafikiri ni kwa nini maji ya chemichemi yalikuwa na mzizimo? (ala.2)
5. Unafikiri hizi zilikuwa sherehe za nini? (ala.1)
6. Eleza tofauti kuu iliyoko baina ya shughuli za wanaking'ozi na zile za Magharibi mwa Kenya. (ala. 2)

7. Eleza maana ya maneno/ vifungu vya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (ala. 3)
i) Kupiga milundi…….
ii) Ngorombwe……..
iii) Imezikwa katika kaburi la sahau……..

2. UFUPISHO.

Soma kifungu kifuatacho ujibu maswali.

Mi-Jadala moto iliyokuwa bungeni majuzi inaonyesha dhahiri kuwa wabunge wetu hawakutaka katika ifanyiwe marekebisho. Kile ambacho hakikueleweka vyema ni iwapo wabunge hawa walifanya hivyo kwa nia njema au la. Huenda walifanya hivyo kwa lengo la kuwa na katiba ambayo itazua mzozo miongoni mwa wakenya ili ikataliwe baadaye ama walifanya hivyo kwa sababu katiba yenyewe ni nzuri na itatufaa kama taifa.

Utata ambao ungali unawababaisha wengi ni mahakama za kadhi, uavya ji wa mamba, ugatuzi wa mamlaka, ardhi na kwamba mawaziri wawe watu mbali na wabunge na mengi. Yale ambayo yanalemea katiba zaidi ni swali la mahakama za kadhi na uavyaji wa mamba. Makanisa, hasa kanisa katoliki, yamesema ni lazima yaangushe katiba hiyo iwapo haitafanyiwa marekebisho.

Swali la uavyaji mamba halishughulikiwa lakini si kumaanisha kwamba uavyaji mamba haukuwepo asilani mada ktari wamekuwa hawajali katu kiapo chao cha utenda kazi kwa uadilifu bali walikuwa wakiweka pesa moele. Hatua hii imekiuka haki za kibinadamu kwani ambazo zimekuwa zikitunguliwa ni za watoto walio na haki ya kuishi kamam mimi na wewe.

Maoni yamekuwa kwamba nyakati nyingine ni sharti uavyaji wa mamba utekelezwa kutokanan na ushauri wa daktari ili kuokoa maisha ya mmoja; mama au motto. Ina maana kuwa endapo kuna dharura na hatua kama hii haichukuliwi itazua hatari kwa wote wawili na huenda wakaangamia.

Katiba ya sasa haisemi chochote kuhusu uavyaji wa mamba japo sote ttuajua kwamba ni msuaji ya kikatili. Enzi hizo jambo hili lilifumbiwa jicho; halikuzungumziwa hata kidogo. Hii ndio sababu kulingana na kielelezo cha katiba ikabainika na kamati ya wataalamu wa katiba (COE) kwamba kuna haja ya kuwepo na kifungu katika sheria kinachodhibiti hali kama kuhalalisha kila uavyaji wa mamba unaofanyika katika hospitali kuwa iikuwa ni dharura ya kuokoa maisha.

Hilo linawaogofya viongozi wa makanisa sana pamoja na waumini kwani kwao linafaa kuwa swala la kimaadili. Daktari na mteja wake sharti wajue kuwa watakuwa na mashtaka ya kujiu mbele za mungu endapo wataamua kuangamiza maisha ya kiumbe kisicho na hatia. Tunalosema hapa ni kwamba hili ni swala la imani zaidi kuliko sheria, liwekwe katika katiba ma lisiwekwe laweza kuendelezwa na watu waliozoea kutenda unyama.

Hatuna haja ya kuizima katiba iliyofikia hatua ya mwisho kutokana na jambo tusiloweza kudhibiti. Tutakuwa kama mtu anayemwaga mapipa kadhaa ya maziwa eti kwa sababu nzi mmoja ametumbukia ndani. Mbona tusimtoe nzi huyo kwa njia safi na tyanywe maziwa yetu.

Tunalopendekeza hapa ni kwamba katiba iacha ne na swala hili ambalo uamizi utakuwa ukafanywa na daktari pamoja ma mteja au jamaa zake. Itaweza kuwa wazi kuwa sheria itawaandama hawa endapo ithibika baaday kuwa walikiuka maadili ya kikazi nay a kijamii.

Vivyo hivyo katika mahakama za kadhi mabzo zimekuwepo tangu jadi. Waislamu hawadhamini kuzitumia sheria hizi kuchukua uongozi wa taifa hili kwa mabavu. Zinashughulikia kesi za kifamilia na zile za nchi hupelekwa katika mahakama zetu za kawaida. Hakika, hii ni pilipili ambayo hatujaila na kwetu hatuoni yatuwashiani.

Ukweli ni kwamba Mahakama za kadhi zimekuwepo hata katika katiba ya awali. Zimekuwa zikishughulikia daawa za kinyumbani ardhi na ndoa katika dini ya kiislamu.

Katiba ni yetu hata ichukue muda zaidi na zaidi. Wanakamati wa COE wapewe idhini na wabunge ili washughulikie baadhi ya maswala yanayodaiwa kuwa nyeti ili yawekwe wazi zaidi. Ukweli ni kwamba hatuwezi kuitupa katiba kwa kuwa itakuwa na hasara kubwa na vizazi vijavyo.

Maswali

A. Eleza utata uliopo tunaposhughulikia uavyaji wa mimba ***(Maneno 50)*** (ala. 6)
B. Kwa kutumia maneno yasiyozidi arobani fupisha aya tatu ya mwisho. (ala.6)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a. Akifisha

Una kiberiti yule mtu aliniuliza na nilipotoa kiberiti na kuwasha yule mtu alinizaba kofi maria alieleza

b) Taja sauti nne za konsonanti ambazo ni za nasali. (ala.2)

c)Tunga sentensi inayodhihirisha mstumizi ya ngeli ya I – ZI. (ala 2)
Umoja…….
Wingi……..
d) Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo. (ala.2)
i)Nafsi ya tatu umoja…….
ii) Hali timilifu…….
iii) Kitendwa…….
iv) Mizizi……..
v) Kiishio…….
e) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (ala.5)
sikumwadhibu kwa sababu alikuwa mgonjwa.
f) Neno mlevi limetumikaje katika sentensi zifuatazo? (ala.2)
i) Mlevi alosababisha ugomvi……..
ii) Mtu mlevi alisababisha ugomvi……..
g) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii. (ala.2)
Nitaenda nyumbani ingawa ninaumwa na kichwa
h) Tunga sentensi sahihi ukitumia <u>hadi</u> kama: (ala. 2)
i) kihusushi cha wakati…….
ii) Kihusishi cha mahali……
i) Eleza matumizi ya kwa, ka, na ku katika sentensi zifuatazo. (ala 3)
i)Nita<u>ku</u>taka ufika hapa……
ii) <u>Ka</u>chezeni kule nje……..
iii)Yule utaalamu alielezea maana ya utandawazi <u>kwa</u> ufasaha…….
j) Ziandike sentensi zifuatazo kwa kuzingatia maagizo. (ala. 2)
i) chakula kinachoiva vizuri ndicho kinacholiwa **(hali ya mazoea)**
ii) Timu ile imeshinda. Haikucheza vizuri **(Tujmia ijapokuwa)**
k) Sentensi hizi ni za aina gani? (ala 2)
i) Mkulima aliyekata nafani atasaidiwa kesho……..……
ii) Walimu na wazazi wanatengeneza bweni……
l) Andika kinyume cha: (ala. 2)
i) Mtweke Bi. Kizee mtungi huu wa maji.
ii) Mama alitandaza zulia kubwa sebuleni.
m) Tumia vitenzi – nya na ja kutunga senstensi sahihi katika kauli ya kutendewa. (ala 2)
n) Andika kwa msemo halisi. (ala 2)
Wanga alisema kuwa alikuwa amepata alama zote katika mtihani wa mwisho wa mwaka.
o) Andika kwa wastani halafu kwa ukubwa . (ala. 2)
Kibuzi kile kimono kina kiguu kinachouma.
p) Andika kwa wingi: (ala 2.)
Kuku yuyu huyu ndiye aliyetaga yai hili.
q) Yakinisha sentensi hii. (ala 1)
Usipolala sana hutapona haraka.
r) Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo kubainisha maana. (ala. 2)
i) Bana
ii) Pana.

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)
a) Eleza maana ya mitilinguo . (ala.1)
b) Huku ukitoa mifano halisi eleza tofauti iliyopo baina ya kuchanganya ndimi/ misimbo na kubadili ndimi/misimbo (ala. 4)
c) Eleza sababu tano za kuchanganya na kubadili misimbo /ndimi. (ala. 5)